

KUSOMA KULINGANA NA SHERIA YA GREDI YA TATU

Mwongozo wa Wazazi wa Sheria ya 306 ya Umma



Ingham Intermediate
School District
A Regional Educational Service Agency

1 Je, Sheria Hii Inahusu Nini?

- ▶ Katika juhudi za kuboresha mafanikio ya kusoma, wabunge wa Michigan walipitisha Sheria ya 306 ya Umma Mnamo Oktoba 2016.
- ▶ Ili kuwasaidia wanafunzi zaidi kuweza kuandika na kusoma mwisho wa gredi ya 3, sheria inahitaji usaidizi wa ziada kwa wanafunzi wa K-3 ambao wanashindwa kusoma katika kiwango cha gredi.
- ▶ Sheria pia inasema kwamba mtoto anaweza kusalia katika gredi ya 3 ikiwa yuko nyuma katika kiwango kimoja au viwango zaidi vya gredi katika kusoma mwisho wa gredi ya 3.

2 Ni nini Kingine Ninahitaji Kujua Kama Mzazi?

- ▶ Maendeleo ya kusoma ya mtoto wako yatafuatiliwa kwa karibu katika shule ya chekechekeka.
- ▶ Ikiwa mtoto wako hasomi kulingana na anavyotarajiwa, mpango wa kuboresha kusoma kwake utaundwa.



Hii inamaanisha mwalimu na shule ya mtoto wako watafanya kazi pamoja na mtoto wako ili kufahamu ni wapi mtoto wako anahitaji usaidizi katika maendeleo yake ya kusoma na kuunda mpango wa kumsaidia. Mpango huu unajumuisha:

- ▶ Masomo ya ziada au usaidizi katika maeneo yanayohitaji usaidizi.
- ▶ Kaguzi zinazoendelea kuhusu maendeleo ya kusoma
- ▶ Mpango wa kusoma nyumbani ambao unakuhimiza wewe na mtoto wako kusoma na kuandika nje ya siku ya shule.
- ▶ Mtoto wako anaweza kuhimizwa kushiriki katika mipango ya kusoma ya majira ya joto.

- ▶ Usaidizi wa ziada katika mpango wa kuboresha kusoma kwa mtoto wako utafanyika katika makundi madogo wakati wa siku ya shule. Mtoto wako hatakosoma masomo ya kawaida ya kuandika.
- ▶ Kuanzia mwaka wa masomo wa 2019-2020, ili kupandishwa darasa kutoka gredi ya 3 hadi ya 4, lazima mtoto wako apate alama zaidi kuliko mwaka uliopita katika mtihamu wa kusoma wa jimbo, au aonyeshe kiwango cha kusoma cha gredi ya 3 kupitia mtihamu mbadala au ripoti ya kazi ya mwanafunzi.
- ▶ Ukiarifiwa kuwa mtoto wako ataendelea kusalia, una haki ya kukutana na maafisa wa shule na kuomba, ndani ya siku 30, kukubaliwa ikiwa itakuwa kwa manufaa ya mtoto wako. Msimamizi wa wilaya atatoa uamuzi wa mwisho.

3 Je, Ni Nini Ninachoweza Kufanya Ili Kumsaidia Mtoto Wangu?

Soma nyumbani na mtoto wako vitabu ambavyo anavifurahia katika msimu wa joto. Baadhi ya njia za kufanya hivi:



- ▶ Msomee kwa sauti mtoto wako.
- ▶ Msikilize mtoto wako akisoma.
- ▶ Kusoma kimkakati (Unasoma mstari, kisha anarudia).
- ▶ Someni pamoja kwa wakati mmoja.
- ▶ Soma tena au simulia tena hadithi azipendazo.
- ▶ Ongea na mtoto wako kuhusu kusoma.

Wasiliana na mwalimu wako mkuu wa uwezo wa kufanya kazi pamoja kwa maelezo zaidi na usaidizi wa mtoto wako.

Tazama video hii kuhusu jinsi ya "KUSOMA" na mtoto wako na ujaribu nyumbani: <https://youtu.be/FjJDIUDwVKg>

Unapokuwa ukisoma:

- ▶ Muulize mtoto wako ashiriki anachokumbuka.
- ▶ Uliza maswali kuhusu kusoma.
- ▶ Ongea kuhusu sehemu zako unazozipenda, ulichojifunza, au ni nani yuko kwenye kitabu na anachokifanya.
- ▶ Ongea kuhusu picha katika kitabu na jinsi zinavyoshirikiana na maneno kwenye ukurasa.
- ▶ Saidia kuhusisha hadithi na maisha ya mtoto wako au vitabu vingine ulivyosoma



- ▶ Ongea na watoto wako zaidi – kujua maneno zaidi huwasaidia watoto kuelewa maneno wanayoyasoma vizuri zaidi.
- ▶ Himiza kuandika – Waruhusu watoto kuandika sauti wanazozisikia, tahajia ni ustadi wa kukuzwa na kuendelezwa.
- ▶ Husika katika elimu ya mtoto wako na uunge mkono mpango wa kusoma ikiwa mtoto wako anao.

Tazama shughuli hii ya kusoma na ujaribu nyumbani na mtoto wako:

Kusoma Kimkakati:

<http://bit.ly/2dUEDPI>

